



KAMATI YA SIASA MKOA WA SIMIYU YARIDHISHWA NA UTEKEREZAJI WA MIRADI ITILIMA



Mwenyekiti wa CCM Mkoa Mhe. Mzee Enock Yakobo wa Pili Kutoka Kushoto akipokea maelezo ya Maendeleo ya Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Itilima kutoka kwa Eng. Wa Halmashauri ya Itilima Ndg. Furaha Mwampulo wakwanza kulia katibu mwenezi wa CCM Mkoa, akifuatwa na Mwenyekiti wa UWT Mkoa Mama Manyangu

Kamati ya Siasa Mkoa ikiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Simiyu Mzee Enok Yakobo yafanya ziara ya Kustukiza Wilayani Itilima kwa lengo la Kukagua na Kuji-ridhisha na utekerezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Wilayani humo.

Kamati hiyo Ikiwa Makao Makuu ya Wilaya ya Itilima ilipendezwa na Hatua nzuri ya Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi awamu ya pili na Kwa gharama nafuu ya shilingi Milion milioni 331 linalo jengwa kwa mfumo wa “Force Account”, ikilinganishwa na awamu ya kwanza ambayo ilijengwa na Mkandarasi ambaye ni Wakala wa Majengo

Tanzania (TBA) kwa gharama ya Shilingi Milioni 670 fedha za Serikali.

Mzee Enock Yakobo alisema “kwa kweli Itilima Hamjawahi kuniangusha siku zote Mmekuwa mkifanya vizuri na ndiyo maana Mimi na Kamati yangu tukaamua tuanzie Itilima ili tuanze Siku yetu Vizuri”

Aidha Kamati hiyo Ikiwa Katika Kata ya Migato kwa Lengo la kukagua Jengo la Wodi ya Wazazi katika Zahanati ya Migato iliyojengwa kwa ghalama ya shs. Milioni 30 kutoka UNFPA, ilimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itilima Kuboresha Zaidi huduma zinazotolewa Kituoni hapo ili kuondokana na hali ilivyo ivi sasa

Akiahidi kuyafanyia kazi maoni ya Kamati hiyo Kai-mu Mkurugenzi Ngd. Keli-sa Wambura aliiomba kamati hiyo kukumbusha ahadi iliyo tolewa na Nambu Waziri wa Afya Mhe. Dkt. Faustine Ndungulile ya shs milioni 400 aliyo ahidi kuipatia Zahanati ya Migato kwa lengo la kuanza mchakato wa ujenzi wa Kituo cha Afya ili kukabariana na wingi wa watu waopata huduma katika Zahanati hiyo.

Inaendelea uk 4



Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Simiyu wakiongea Wateja wanao subiri huduma ya Tiba katika Zahanati ya Migato iliyopo wilayani Itilima



Kamati ya Siasa ya mkoa chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wakishuhudia uwekaji wa Jamvi katika ujenzi wa j Jengo la Utawala la Hospitali ya wilaya ya Itilima



Jengo la ofisi ya Mkurugenzi wa Halmshauri ya Wilaya ya Itilima (ujenzi wa awamu ya pili) likiwa katika Muonekano wa kuelekea katika hatua za mwisho za ukamirifu.



Kamati ya Siasa ya Mkoa chini ya Uongozi wa Mhe. Mzee Enock Yakobo ikiwa katika eneo la bwawa ya Mwapalala nakuhoji baadha ya kasoro zilizopo katika Bwawa hilo wakwanza kulia Kaimu Mkuu wa Idara ya Maji Eng. Emanuel Mafuru



Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa Mhe. Mzee Enock Yakobo akimsikiriza Fundi Kiongozi wa ujenzi wa Jengo la wodi ya Wazazi katika eneo la ujenzi wa Hospital ya Wilaya ya Itilima.

Kamati ilijielekeza katika Kijiji cha Nguno, kilichopo katika Kata ya Lagangabilili kwenye mradi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Itilima iliyotengewa pesa na Serikali kiasi cha Shs. Bilioni 1.5 kujionea maendeleo ya ujenzi unaohusisha majengo sita ikiwemo Wodi ya Wazazi, Jengo la Utawala, Jengo la Kufulia, jengo la Kuhifadhia Madawa (Famarcy), Maabara na Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD).

Katika ujenzi huo Mwenyekiti wa CCM Mkoa Mhe. Enock Yakobo alimtaka Eng. Wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima Furaha Mwampulo kuhakikisha mafundi wake wanaongeza kasi kwa lengo la Mradi kumalizika kwa wakati, lakini bila kuathiri Ubora wa Majengo, pamoja na Kumtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itilima kuhakikisha anatatua changamoto zote zinazo kwamisha Ujenzi huo kuendelea

kwa kasi inayo takiwa.

Vilevile Kamati ilielekea katika Kata ya Nkoma kukagua Mradi wa Mabweni mawili ya watoto wa Kike katika shule ya Sekondari Nkoma ambapo Bweni moja katika mradi huo lilipata ufadhiri kutoka Ubarozi wa Watu wa China wa Shs milioni 178, Mradi wa Ujenzi wa Bwalo la Chakula na Ujenzi wa Madarasa Mawili kwa fedha kutoka serikalini kiasi cha tShs million 140/.

Katika Mradi wa Bweni la pili ambalo limejengwa kwa nguvu ya Wananchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi Mhe. Enock alimtaka Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itilima Mhe. Daudi Nyalamu kuhakikisha ujenzi huo

unakamilika mapema iwezekanavyo kabla ya ugeni unaotarajiwa kuja ukimuhusisha Barozi wa Jamhuri ya Watu wa China Nchini Tanzania.

Kamati ilihitimisha Ziara yake katika kata ya Mwamapalala na Kukagua Mradi wa ukarabati wa Bwawa la Maji la Mwamapalala ambalo limeghalimu kiasi cha pesa Zaidi ya shs. Milioni 600 maoni ya kamati yaliyo tolewa na Katibu wa CCM Mkoa Mhe. Mayunga George yaliitaka Ofisi ya Mkurugenzi kurekebisha baadhi ya kasoro zilizojitokeza ikiwepo uondoaji wa Magugu maji ambayo yanaenea kwa kasi na kuli-funika Bwawa hilo.



Mtendaji wa Kata Nkoma Bi Alphoncina Oswald Rusasa akitoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa Madarasa Katika shule ya Sekondari Nkoma